# *Siku Ya Maombi ya Amani kwa ajili ya Yersusalemu*

## ***JumaPili ya Kwanza ya Kila Oktoba***

### Kweli Muhimu Kuhusiana na Siku ya Maombi ya Amani kwa ajili ya Yerusalemu

## NI NINI HIKI?

*Siku ya Maombi ya Amani kwa ajili ya Yerusalemu ya ki-mataifa, iliasisiwa na jumuiko la viongozi wa makanisa na Huduma za Ki-kristo zaidi ya 1300 toka katika madhehebu na tamaduni mbalimbali za dunia, maombi haya* ***yatafanyika Jumapili ya kwanza ya kila Oktoba.***

*Wito wetu ni kuuhimili, kutia hamasa ya maombezi na kuutaarifu ulimwengu juu ya mipango na makusudi ya Mungu kuhusu Yerusalemu na watu wake wote. Huu mchakato na chanzo cha maombi ya ki-limwengu unashaabiana na majira ya Yom Kippur, na kwa mara ya kwanza katika historia, panafanywa jitihada katika kuziunganisha ki-lutlujia kalenda za Ki-kristo na ile ya Ki-biblia, yaani kalenda ya Kiyahudi.*

**Hiki chanzo cha Maombi Ki-limwengu kiko chini ya Wenyeviti wenza Dr. Jack** Hayford (Rais wa Makanisa ya Foursquare na Chancellor wa The King's University) **na Rev. Robert Stearns** (Muasisi na Mkurugenzi Mkuu wa Huduma ya Eagles' Wings.)

## LITAFANYIKA LINI?

Siku ya Maombi ya Amani kwa ajili ya Yerusalemu itazingatiwa kila Jumapili ya kwanza ya Octoba, karibu na majira ya Yom Kippur. ***Mwaka huu – 2012 – itaangukia tarehe 7 Oktoba.***

## NANI ATASHIRIKI KATIKA HILI?

- Makumi ya Mamilioni ya Wakristo, toka tamaduni mbalimbali, madhehebu na vizazi, toka makanisa makuu ya ki-dayosisi katika miji yote duniani kwa ngazi ya makanisa yasemayo lugha za asili toka Africa na hata makanisa yasiyodhahiri katika mataifa ya Ki-islamu.
- Mwaka 2011 tulikuwa na mataifa zaidi ya 175 yaliyojumuika – **ikiwa ni pamoja na makanisa 7 yasiyodhahiri toka mataifa ya Ki-islamu** – na mwaka huu wa 2012, kwa neema ya Mungu tunatumainia takriban mataifa mengi kushiriki katika kuiombea amani kwa ajili ya Yerusalemu.

## INAZINGATIWAJE SIKU HII MUHIMU?

- ***Ki-msingi, kuomba kwa ajili ya amani ya Yerusalemu kwapasa kufanyika katika kila ushirika wa kanisa la mahala kama sehemu iliyofungamana na ibada tarehe 7 October.*** *Kushiriki katika DPPJ kwaweza kuwa kwa namna ya kawaida kwa kuyatumia machapishi yaliyopachikwa kanisani huku programu zikiendelea ,na katika kuzihusisha jumbe & baadhi kujitoa kwa maombi siku hii ya tarehe 7 Oktoba, au, kwa kadri itakavyoshirikishwa kwa ilinganifu wa Muda kwa namna kila kanisa lionavyo vema. Kilicho muhimu ni kuwa, tunataka kila aina ya makanisa, toka katika kila ibada mbali mbali, toka Marekani yote, washirikiane na wakristo kote duniani kuomba kwa ajili ya amani ya Yerusalemu, kwa viwango vyao vya uelewa uhusuo hitaji la mkakati.*
- *Baadhi ya miji, majimbo au mataifa pia yanafanya makusanyiko ya ki-majimbo –katika kuambatanisha ibada –ili kudhihirisha umoja katika maombi kwa ajili ya amani ya Yerusalemu na watu wake.*
- *Kadhalika, tunalo vuguvugu linalokuwa katika eneo la shule, ambalo huwakuza wanafunzi wanazuoni wakristo toka kila kona za Dunia, ili kuwa masalia/mabaki na kuwakilisha shule zao Oktoba 7kwa kuomba Baraka za Mungu juu ya ardhi hii iliyo na utata na watu wake. Tazama www.daytopray.com.*
- *Panapo siku maalumu ya kusanyiko la Maombi huko Yerusalemu na viongozi wa makanisa toka kote duniani na waheshimiwa toka Israeli watakaorushwa papo kwa papo katika God TV kwa zaidi ya mataifa 200 siku hiyo.*
- *Pia, yapo masaa 24 ya Congamano la Maombi kwa njia ya simu, chini ya usimamizi wa Wito Mkuu (*www.greatercalling.org)*ambapo watu toka kote duniani , kila kanda zenye tabaka za mida tofauti, zinaweza kupiga simu zao katika "chumba cha maombi cha papo kwa papo" kwa simu zao na maombi ya pamoja kwa ajili ya mahitaji mengi ya mkakati huu wa ki-majimbo na makundi yao ya watu.*

## NITAZIPATAJE TAARIFA ZAIDI?

Tafadhali bofya katika www.daytopray.com kwa ajili ya yafuatayo:

- Nyenzo za Tafsiri za Siku ya Maombi, Machapishi, Jumbe, nk. Katika lugha mbali mbali, inayoweza kupatikana ki-mtandao &/au kudurufiwa katika comyuta. Tunavyo vyanzo vilivyotafsiriwa katika lugha 29 tofauti tangu mwaka jana, zikiwa katika Tovuti zetu na tutazifanyia mabadiliko kila ipasapo na kuongeza tafsiri za ziada katika mwaka.
- Tunazo tayari Programu za DPPJ za watoto wa umri wa 3-5, na 13-18, vijana wa umri kati ya 13-18 zilizodurufiwa katika lugha ya kingereza. Hizi ni pamoja na lesoni, kazi za sanaa, kurasa zilizotiwa rangi, na kadi za maombi.
- PSAs (Public Service Announcements) yaani vipaza sauti katika hadhara na Video
- Machapisho ya Waandishi
- Orodha ya Viongozi kote duniani wakihamasisha wito wa kuomba
- Orodha ya ki-jimbo, ki-taifa, na waratibu wa ki-mataifa wahamasishao vuguvugu la Maombi haya na taratibu za kuwasiliana palipo maswali.
- Vyanzo na vifaa ambavyo vinaweza kuagizwa ili kulikamilisha kanisa au kikundi cha Mafunzo ya Biblia ya kuuwezesha utekelezaji wako wa Oct. 7
- Picha na maelezo ya watekelezaji wa maombi wa miaka iliyopita

- Historia ya Siku ya Maombi kwa ajili ya Amani ya Yerusalemu

Kadhalika, unaweza kupiga simu ofisi ya Eagles' Wings kupitia na 716-759- 1058 au 1-800-51WINGS

## NITAHUSIKAJE?

Unaweza kuwasiliana na mratibu wako wa Mkoa, Jimbo, au taifa kupitia webpage ya mratibu wetu palipo na uwezekano wa kumtumia barua pepe moja kwa moja kwa majina yao.

Ikiwa taifa lako, mkoa, au jimbo halina mratibu wa DPPJ, unaweza kuwasiliana nasi kwa njia ya tovuti www.daytopray.com au tupigie simu ya ofisi na 1-800-51 WINGS.

## JE, KUOMBA KWA AJILI YA AMANI YA YERUSALEM KUNANIMAANISHA KUWA KINYUME CHA WAARABU NA WAPALESTINA?

Mungu siyo mwenye kumweshimu wanadamu; Huwapenda wote kwa usawa. Anao mpango wa ukombozi kwa ajili ya uzao wa Isaka na uzao wa Ishmaeli. Tunapoombea amani ya Yerusalemu, tunawaombea watu WOTE wa makazi hayo. Kusudi ya mioyo yetu ikitazamia kuliona neno la Mungu likitimia. Tunataka kuuona ule ukuta wa matengano kati ya Wayahudi na Waaarabu ukivunjwa (Efe. 2:14), tuuone umoja, upendo na shukrani za kurejeshwa kwa kila mmoja, na utimilifu wa Shalom/Amani na Baraka vikijikita juu ya ardhi na watu wake.

## KWA NINI NIOMBE KWA AJILI YA AMANI YA YERUSALEMU?

- **Mwanzo 12:3 –***Bwana anasema katika agano alilolifanya na Abrahamu:* ***"Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa." Kwa udhahiri, Historia inatuthibitishia kuwa mataifa na viongozi waliowabariki Israeli na Wayahudi walibarikiwa kipekee na Mungu, na wao waliowalaani Wayahudi na ardhi yake takatifu nao wakawa katika ghadhabu ya Mungu.***

- **Mungu akawavuvia waandishi wa maandiko kuandika kisicho kikomo wala badiliko kwa kila amfuataye yeye kuomba *"Utakieni Yerusalemu amani; na wafanikiwe wakupendao;" (Zaburi 122:6).***

- ***Yerusalemu – na taifa la Israeli – ndiyo demokrasia pekee (yenye uhuru wa kidini na haki kwa watu wote na jinsia zao katika mwambao mzima wa nchi 22 za Uharabu zisizo za ki-demokrasia.*** *Israeli na Marekani kwa pamoja ni watetezi wa uthamani na uhuru dhidi ya adui husika, yaani Waislamu wenye mlengo mkali.*

- **Tunawiwa na Wayahudi deni lisiloelezeka la shukurani kwa ajili ya msingi wa imani ya ki-kristo waliouweka na mchango wao usioelezeka katika kuiinua jamii kwa madawa, kilimo na makuzi makubwa ya kiteknolojia.**

- **Ni wajibu wa kanisa kusimama na watu wote wenye agano la kuirejesha Israeli na malengo yake katika ardhi husika.** *Huu ni Wajibu wa Wakristo Kulikamilisha Neno la Kiunabii kwa Wayahudi na kizazi chao.*

- **Historia ya kanisa inathibitisha wingi wa mateso dhidi ya Wayahudi, yaani, *yale yafanywayo kama taswira ya jina la Kristo lakini siyo tabia ya Kristo. Tunao wajibu, katika siku zetu kuyafanya sawa yale yaliyokosewa na Wazee wetu-Wakristo wa zama hizo na kwa nguvu zote, kumwomba Mungu Baraka juu ya ardthi hii na watu wake.***